Kijitabu: Mashirika yasiyo ya faida

**Kufuata sheria mpya**

*Tarehe 1 Novemba 2012, sheria ya mashirika yasiyo ya faida ya 1981* itabadilishwa na *sheria ya madiliko ya Mashirika yasiyo ya Faida ya 2012*. Sheria mpya inajumuisha ' mpangilio wa mda' kusaidia mashirika kuweza kuzoea sheria mpya. Sheria hizo zimeelezwa hapa chini.

## Hadhi ya shirika lisilo la faida

Shirika lisilo la faifa liloandikishwa chini ya sheria ya zamani litaendelea kutambuliwa chini ya sheria mpya. Tarehe ya kuandikishwa haitaathiriwa na cheti cha kuandikishwa kitaendelea kuwa halisi.

## Malengo ya mashirika

Baada ya sheria mpya kuanza, malengo ya sheria mpya ya mashirika yataweza kutambuliwa kama sheria.

Shirika ambalo litatafuta kuweza kusajiliwa kwa mara ya kwanza baada ya sheria mpya kuanza halitahitaji kujaza fomu ya 'Malengo ya mashirika' , lakini ni lazima litaweka malengo yake kufuata malengo mapya.

Kama shirika litaomba kubadilisha sheria zake baada ya sheria mpa kuanza , malengo yake lazima yajumuishe sheria mpya zilizopendekezwa.

## Sheria

Kipengere cha 1 cha sheria mpya kinajumuisha malengo mapya ambayo mashirika mapya lazima yayaelezee . Haya ni:

- jina la shirika na malengo
- haki za wanachama na majukumu
- taratibu za kujiuzulu na kukoma uanachama
- mchakato wa uteuzi na ukomo wa katibu
- kuandaa na kutunza kumbukumbu za mikutano ya jumla na mikutano ya kamati
- utoaji kwa ajili ya wanachama kupata taarifa ya mikutano ya jumla, ikiwa ni pamoja na taarifa za fedha zilizowakilishwa kwenye mkutano wa watu wote
- haki ya wanachama kupata (kama ipo ni maalum katika sheria) taarifa ya mikutano ya kamati.

Kama shirika linatumia sheria yake yenyewe au sheria mpya, haina haja ya kukimbilia kubadilisha na sheria mpya.

**Mashirika yanayotumia sheria zake zenyewe**

Kama chama kinatumia **sheria yake chenyewe** (yaani, si mfano washeria), sheria zilizopo zitaendelea kuwa halali mpaka zikibadilishwa. Mara wanachama wakiamua kufanya mabadiliko yoyote ya sheria zilizopo, sheria mpya lazima pia kushughulikia kila kitu kinachotakiwa katika kipendere cha 1. Wakati huo huo, kama kuna kutofautiana kati ya sheria za chama hicho na Sheria mpya, mahitaji ya Sheria mpya yatatakiwa kufuatwa.

**Mashirika yanayotumia sheria za muda**

Mashirika haya lazima yapitie sheria mpya ili yachunguze kama inaendana na malengo yao . Kama mashirika hayatajulisha ofisi ya Consumer Affairs Victoria kuhusu sheria zao ndani ya **miezi 12** baada ya sheria mpya kuanza, sheria zao za sasa zitabadilishwa moja kwa moja na sheria mpya.
Kama shirika likijulisha Consumer Affairs Victoria, linaweza:

- Kubadilishia kwenye sheria mpya mapema
- Kuandaa sheria zake mpya.

Kutoka 1 Novemba 2012, tafuta sheria mpya kwenye consumer.vic.gov.au/forms.

Sheria za shirika (zinaweza kuwa za shirika binafsi au sheria mpya) lazima zielezee vipengere vyote vinavyotakiwa chini ya kifungu cha 1. Kama hawatafanya hivyo, umuhimu wa kipengere hicho katika sheria mpya kitachukuliwa kuwa kimemezwa na sheria mpya .

Kwa habari zaidi kuhusu jinsi ya kubadilisha sheria, tazama kijitabu **sheria za mashirika**.

## Afisa wa Umma kubadilishwa na katibu

Chini ya Sheria mpya, neno 'afisa wa umma' limebadilishwa na 'katibu'.

Nyaraka zozote zilizothibitishwa na afisa wa umma chini ya sheria ya zamani hazitoathirika.

Mara baada ya sheria mpya kuanza, katibu anaweza kuendelea au kukamilisha kazi yoyote iliyoanzishwa na afisa wa umma. Consumer Affairs Victoria itachukulia kuwa hii ni mtu yuleyule isipokuwa ukiambiwa vinginevyo.

## Taarifa za fedha

Sheria mpya itaanzisha mfumo mpya wa hatua tatu wa kutoa taarifa. Shirika litaweza kuchukuliwa kama hatua ya kwanza, ya pili au tatu kutegemeana na mapato yake. Kwa mfano:

- Hatua ya Kwanza: $0 - $250,000
- Hatua ya Pili: $250,000 - $1,000,000
- Hatua ya tatu: zaidi ya $1,000,000.

Mfumo huu unachukua njia za zamani ‘ulioelezeka’ na ‘usioelezeka’ .

Mashirika yasiyo ya faida lazima yaelewe mfumo mpya na kuelewa ni hatua ipi inaikumba , maana hii itaathiri kutoa taarifa kwao. Tembelea consumer.vic.gov.au/associations kwa habari zaidi.

**Njia mpya ya kuwakilisha taarifa ya pesa**

Consumer Affairs Victoria itatuma fomu mpya ya kila mwaka kwenye mashirika zikiwa na tarehe za mwisho wa mwaka siku ya au 1 Novemba 2012.

Mashirika yenye tarehe ya mwisho wa taarifa ya pesa kabla ya 30 Juni 2013 wana uamuzi wa kuwakilisha taarifa yao ya mwaka katika fomu mpya au fomu ya zamani ‘iliyoelezeka/isiyo-elezeka’ . Tazama sehemu inayofuata kwa maelezo zaidi.

Katibu (zamani Afisa wa umma) anawajibika kuwakilisha taarifa ya kila mwaka kwa Consumer Affairs Victoria

Badala ya kutuma taarifa ya kila mwaka mwezi mmoja kabla ya tarehe ya mwisho wa mwaka wa fedha wa chama hicho, Consumer Affairs Victoria sasa itatuma baada ya **mwezi mmoja**. Chama kitapata muda wa **miezi mitano** kuanzia tarehe yake ya fedha ya mwaka na kuwakilisha taarifa ya mwaka

Kwa habari zaidi juu ya jinsi ya kuandaa na kuwakilisha ripoti ya mwaka, tazama kijitabu: **Mzunguko wa mwaka na taarifa za fedha.**

**Njia za kuwakilisha taarifa**

Shirika lolote lisilo la faida chini ya sheria ya zamani linaweza kuchagua kuandaa na kuwakilisha taarifa kufuata sheria ya zamani , lakini kwa mwaka wa fedha wenye tarehe *kabla ya* 30 Juni 2013.

Kwa mfano, shirika lenye mwaka wa fedha kutoka 1 Januari 2012 mpaka 31 Desemba 2012 linaweza kuchangua kuwakilisha taarifa ya fedha chini ya hatua mpya au mfumo wa zamani ‘unaoelezeka/usiolezeka’ .

Shirika lenye mwaka wa fedha unaoishia tarehe ya au baada ya 30 Juni 2013 lazima iwakilishe taarifa ya fedha chini ya mfumo wa hatua mpya.

Kama shirika likiwakilisha taarifa ya pesa ikitumia mfumo wa ‘inayoelezeka/isiyoelezeka’ , katibu inabidi awasiliane na Consumer Affairs Victoria ili kuwakilisha fomu, likieleza kama shirika litatoa taarifa kwa mfumo unaoelezeka au usioelezeka kwa mwaka wa ripoti wa 2012-2013.

## Michakato inayoendelea

Kama shirika limefanya maombi yoyote chini ya sheria ya zamani ambayo bado hayajakamilika kabla ya sheria mpya kuanza, yanachukuliwa kuwa yamefanywa chini ya sheria ya mda yaani sheria mpya.

Consumer Affairs Victoria itaweza kushughulikia maombi mengi yaliyowakilishwa chini ya sheria ya zamani bila kuhitaji habari zaidi. Hata hivyo, tutaweza kujulisha shirika husika kama tunahitaji habari zaidi.

Azimio lolote,  miadi, au ilani iliyofanywa chini ya Sheria ya zamani inachukuliwa halali chini ya Sheria mpya.

Hatua zozote zilizochukuliwa na Consumer Affairs Victoria chini ya Sheria ya zamani zinachukuliwa kwa zimefanyika chini ya Sheria mpya.

## Unahitaji habari zaidi?

**Consumer Affairs Victoria**

Consumer Affairs Victoria inaandikisha na kusimamia mashirika yasiyo ya faida katika Victoria, na inasimamia sheria za mashirika yasiyo ya serikali

W: consumer.vic.gov.au/associations

T: 1300 55 81 81

**PilchConnect**

PilchConnect PilchConnect shirika huru, lisilo la faida ambalo hutoa huduma za kisheria za kitaalamu na ushauri kwa vikundi vya kijamii.

W: pilchconnect.org.au

T: 03 8636 4400